NAMNA YA KUTUMIA KITABU HIKI:

1. Anza kila mkutano kwa neno fupi la maombi ukimuomba Mungu kuleta ufahamu kwa washiriki.

2. Soma hadithi kwa washiriki, au ikiwa kunapatikana nakala za kutosha mpate kila mshiriki ili afuatane na wengine pamoja wakati wa kusoma hadithi.

3. Uliza maswali ya mdomo wakati wa mwisho wa hadithi. Makusudi ya maswali haya ni kuangalia na kusaidia pamoja na ufahamu wa hadithi; sio kwa ajili ya mahojiano ya maswali ya Kithiologia.

4. Kutegemea uwezo wa kikundi wa kuelewa hadithi, kwa desturi ni muhimu kurudia kusoma hadithi hiyo tena baada ya maswali.

5. Soma kweli za kiroho. Uwape wanakikundi uhuru wa kukuuliza maswali kuhusu kila kweli ya kiroho. Uwe mwangalifu kamwe usipinge au kuleta mabishano Kwa yeyote. Uwe mwangalifu usije ukaruhusu wao kuuliza maswali ambayo yatawahamisha kwa swala jingine ambalo halihusiani. Ikiwa watafanya hivyo, warudishe

nyuma kwa hoja ya kwanza. Sio lazima kwao kukubali au kupokea kweli za kiroho. Ni muhimu tu kwamba wazielewe kweli hizo kama zilivyofunuliwa katika Neno la Mungu.

6. Uwe na muda ambapo kila mshiriki anapata nafasi ya kushiriki mahitaji na maombi.

7. Omba dhahiri kwa kila mjumbe wa kikundi, kwa jina na kwa mahitaji yote ya maombi. Kama jinsi kundi linavyoendelea, na ikiwa mmoja wao anampokea Kristo, waruhusu kuomba pia kwa wakati huu wa (kuombea wengine) maombezi.

8. Kila siku wakati wa muda wako wa kimya, kumbuka kuomba kwa ajili ya kila mwana-kikundi. Omba kwamba Roho wa Mungu asonge katika maisha yao na kuwaongoza kwenye uamuzi wa kumfuata yeye.

- **Maandiko yote yamenukuliwa kwa ufasaha kutoka Biblia ya tafsiri mpya ya King James. Biblia Takatifu, tafsiri mpya ya King James. © Copyright 1979, 1980, 1982.**

- **Masomo yote yanaweza kunakiliwa bila kuzuiwa kwa vyovyote vile. Hakuna masomo yatakayonukuliwa kwa faida ya kibiashara. © Copyright 1991. junta de missoes nacionais, CBB, Rio de Janeiro, R.J.**

KUZALIWA KWA YESU
MATHAYO 1-2

SOMO LA 1

"Basi vizazi vyote tangu Ibrahimu hata Daudi ni vizazi kumi na vine; na tangu Daudi hata ule uhamisho wa Babeli ni vizazi kumi na vine, na tangu ule uhamisho wa Babeli hata Kristo ni vizazi kumi na vine" Mathayo 1:17

Maria mwanamke Myahudi akawa mjamzito bila ya kuwa na mahusiano ya kimwili kwa kuwa alipata mimba ya Roho Mtakatifu. Mchumba wake, ambaye alikuwa mtu tu wa kawaida, hakutaka kumuaibisha waziwazi, hivyo aliamua kuvunja uchumba kwa siri. Usiku ule ule alipokuwa akifikiri hayo, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto akisema, "Yusufu Mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariam,mkeo maana mimba yake ni kwa uwezo wa Roho mtakatifu.Naye atazaa mwana,nawe utamwita jina lake Yesu,maana Yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao." Maria alikuwa yule mwanamke ambaye nabii Isaya alitabili katika agano la kale wakati aliposema, "Tazama bikira atachukua mimba, naye atazaa Mwana, nao watamwita jina lake Imanueli; yaani "Mungu pamoja nasi!".

Yusufu alipoamka usingizini, alimtii malaika. Akamuoa Maria, lakini hawakuwahi kuwa na uhusiano wa kimwili mpaka alipomzaa mtoto. Yusufu alimwita mtoto yule Yesu kufuatana na maagizo ambayo alikuwa ameyapokea kutoka kwa malaika. Sasa Yesu alizaliwa katika mji wa Bethlehemu, ambao ulikuwa katika mkoa wa Yuda katika nchi ya Uyahuda, na mfalme wa yuda zama hizo aliitwa Herode.

Kulikuwa na mamajusi ambao walikuja kutoka nchi ya mashariki hadi Yuda wakifuata nyota. Kufuatana na masomo yao, nyota hii ilionyesha kwamba mfalme aliyeahidiwa amezaliwa katika Yuda. Bila kujua ni wapi hakika yule mtoto watakapomuona, kwanza walikwenda kwa makao ya Herode, mfalme wa wilaya ya Yuda, na kuuliza ni wapi ambapo mfalme wa Wayahudi amezaliwa.

Herode alifadhaishwa na habari zao na akaita mkutano kwa siri pamoja na viongozi wote na makuhani. Herode akawauliza watu hawa, ni wapi kufuatana na unabii wa Kiyahudi, palikuwa na kuzaliwa yule mfalme wa Wayahudi aliyeahidiwa. Makuhani wakamwambia kwamba kufuatana na Maandiko Matakatifu, mtoto aliyeahidiwa alikuwa azaliwe katika Bethlehemu. Herode akawaendea mamajusi na akawauliza ni lini hakika walipoiona ile nyota kwa mara ya kwanza. Aliuliza hii kwa sababu alitaka kupata muda halisi na tarehe ya mtoto na kupata umri wake.

Herode aliwajulisha mamajusi ni katika mji gani ambapo mtoto angezaliwa. Herode pia alisema, “Nenda na mkamtafute kwa uangalifu yule mtoto mdogo, na mkiisha kumwona, nileteeni habari mimi, ili mimi nami niende nikamsujudie.”

Wale mamajusi kisha wakaondoka mahali pale, wakaendelea kufuata ile nyota hadi Bethelehemu. Ile nyota ambayo walikuwa wakiifuata, ikawatangulia na ikasimama juu ya nyumba mahali ambamo yule mtoto alikuwa. Wakaingia nyumbani mara wakamwona yule mtoto pamoja na Maria, mama yake wakaanguka chini wakamsujudia yeye. Pia walimtolea zawadi zenye thamani za dhahabu, tunu, uvumba na manemane.

Kisha mamajusi wakaondoka mahali hapo kurudi makwao katika mashariki. Lakini kabla ya kuondoka, walikuwa na ndoto ikiwaonya wao kutomrudia Herode na kumwambia jinsi gani ya kumuona mtoto. Hivyo wakaenda zao kwa njia nyingine.

Hao walipokwisha kwenda zao, Yusufu alikuwa na ndoto nyingine. Katika ndoto hii, alikuwa ameonywa na Mungu kwamba Herode alikuwa anakuja kumtafuta mtoto na kwamba wangelazimika kukimbilia Misri. Kwa hiyo, usiku ule ule, aliamsha familia yake na wakakimbia mara moja. Waliishi katika Misri mpaka kifo cha Herode, hii pia ikiwa ni utimilifu wa unabii wa Nabii Hosea ambapo alisema, “Kutoka Misri nitamuita Mwanangu.”

Herode, baada ya kugundua kwamba mamajusi wamemdhihaki, akaghadhabika sana. Ndipo alipotangaza kwamba watoto wote wa kiume chini ya miaka miwili wangeuawa. Ilikuwa ni mauaji ya kutisha ya watoto wote katika Bethelehemu na miji inayoizunguka. Kwa vyovyote vile, nabii mtangulizi Myahudi aliyeitwa Yeremia vilevile alikwisha tabili msiba huu.

Wakati Herode alipofariki, malaika alimtokea Yusufu na kumwambia arudi Israeli. Yusufu, kwa kadiri yoyote, alikuwa kidogo ana wasiwasi kwa sababu mwana wa Herode ndiye alikuwa mtawala wa Yuda. Kwa hiyo alihamisha familia yake hadi mkoa jirani wa Galilaya kwa mji unaoitwa Nazareti. Yesu alitumia muda wake wa utoto katika mji huu. Hii pia ilikuwa ni utimilifu wa unabii uliosema, "Ataitwa Mnazorayo."

MASWALI YA MDOMO

1. Maria ni nani?

2. Yusufu ni nani? Malaika alimwambia nini? Mtoto angeitwa nani?

3. Kwa nini mamajusi walikuja kutoka mashariki hadi Yuda?

4. Kwa nini Herode alitaka kumuona Yesu?

5. Jinsi gani mamajusi walijua kuwa wanapaswa kurudi nyumbani kwa kupitia njia nyingine na kutomrudia Herode?

6. Jinsi gani Herode alijaribu kumuua mfalme wa Wayahudi aliyeahidiwa?

7. Jinsi gani Yusufu alivyojua kuwa analazimika kuikimbia nchi kwenda Misri?

8. Jinsi gani Yusufu alivyojua wakati ulio wa salama kurudi?

9. Ni jina gani la mji ambalo Yesu alitumia muda wa utoto wake?

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 1-2

SOMO LA 1

1. **Mungu ni mwaminifu na daima hutunza ahadi zake.** Tangu kuumbwa kwa mwanaume na mwanamke wa kwanza, Mungu alikuwa ameshaahidi kwamba angemtuma mkombozi kwa ulimwengu. Baada ya miaka, yeye alirudia ahadi hii mara nyinngi kwa watu wengi mara kwa mara na maelezo mengi ya jinsi gani kuja kwake kungekuwa. Yesu alikuja ulimwenguni barabara kama ilivyokuwa imetabiriwa kupitia maandiko Matakatifu. Ebu sisi tukumbuke katika hadithi angalau unabii mmoja ambao ulitimilika kupitia kuzaliwa kwa Yesu.

♦ Mungu ni mwaminifu kwetu sisi katika njia hiyo-hiyo. Katika Biblia, zipo ahadi nyingi muhimu ambazo Mungu ameahidi kuhusu mpango wake, kwa ajili yetu. Ni muhimu kusoma Maandiko Matakatifu na kuzigundua ahadi za Mungu kwa ajili ya maisha yetu.

2. **Biblia ni Neno la Mungu na kila kitu kilichomo ni kweli.** Mungu alisema kupitia kwa manabii miaka maelfu mbele ya maelezo halisi kuhusu kuzaliwa na maisha ya Yesu. Kila kitu

kilitokea sawasawa kama ilivyokuwa imetabiriwa na manabii.

3. **Mungu ni mtawala wa vitu vyote.** Yeye ndiye anayefanya vitu vitokee ambavyo ni maajabu na miujiza. Kuna vitu baadhi vya ajabu au miujiza ambavyo vilitokea katika hadithi hii. Ni vipi kati ya hivi?
4. **Mungu anaweza na huwasiliana na watu.** Baadhi wanaamini kwamba Mungu aliumba ulimwengu lakini hajali ni nini kinachotokea hapa. Ni njia ipi ambayo Mungu aliitumia kuwasiliana na watu katika hadithi hii? Mungu bado anawasiliana na sisi hata leo hii. Tutajifunza kupitia somo hili jinsi gani sisi tunaweza kuwa na uhusiano halisi na Mungu.

5. **Mungu anajua kila kitu kinachoenda kutokea; lakini mara nyingi, katika hekima yake ya Ki-Mungu huwa anaruhusu vitu vya kutisha vitokee.** Herode alitaka kumuua mfalme aliyeahidiwa kwa sababu alimuogopa Yesu. Mungu alijua dhambi mbovu katika moyo wa Herode. Yeye alijua kwamba Herode alikuwa anakwenda kuwaua mamia ya watoto wasio na msaada. Kwa sababu ya kutotii na maasi katika moyo wa Herode hofu kubwa ikatokea. Leo hii, mara nyingine, vitu vya kutisha huwa vinatokea kwa sababu ya kutotii na maasi katika maisha yetu. Je, wewe unajua mfano wa kisasa ambapo mtu mmoja ameumizwa kwa sababu ya uovu wa mtu mwingine?

6. **Mwanadamu kamwe hawezi kushindana na Mungu na kushinda.** Herode alikuwa hawezi kumuua mtoto aliyeahidiwa. Kitu pekee alichotimiza vizuri ilikuwa ni kutengeneza msiba wa kutisha katika maisha ya familia nyingi. Leo hii, muda wetu mwingine, tunajaribu kutotii sheria za Mungu na mapenzi yake. Hii kila mara huleta msiba, ikiwa sio kwetu sisi ni kwa wale wanaotuzunguka ambao ndio tunawaumiza. Je, unaweza kufikiria juu ya wakati katika maisha yako binafsi ambapo ulifanya kitu kibaya na kikaleta msiba katika maisha yako? Je, unaweza kufikiria juu ya wakati Fulani wakati uliumizwa kwa sababu ya maasi ya mtu mwingine?

7. **Mapadri na washauri wa kidini walijua Maandiko Matakatifu kuhusu aliyeahidiwa lakini hawakwenda kukutana na Yesu.** Je inawezekana kuwa mwanadini; kujua mengi kuhusu Biblia, kujua mengi kuhusu Yesu Kristo, lakini **kamwe si rahisi kujua ndani ya moyo wa mtu?**

8. **Yeye ni "Mungu pamoja nasi" au "Imanueli."** Malaika alisema maneno haya kwa Yusufu, ambayo yalinukuliwa katika Maandiko Matakatifu na nabii Isaya. Watu wengi wanasema kwamba Yesu alikuwa nabii, wengine wanasema kwamba Yesu alikuwa malaika au mtu mwema. Lakini Biblia hutufundisha sisi kwamba Yesu alikuwa "Mungu pamoja nasi."

Katika majuma sita yafuatayo, tutakwenda kujaribu, kugundua hakika Yesu Kristo ni nani, na ni nini Habari Njema ambayo aliileta ulimwenguni.

KUBATIZWA KWA YESU
MATHAYO 3-4

SOMO LA 2

"Tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia." Mathayo 3:2

MARUDIO:

1. Jina la mama yake Yesu lilikuwa _____.

2. Muujiza mmoja uliozunguka kuzaliwa kwa Yesu ni kwamba alizaliwa na _____ _.

3. Agano la Kale lilitaja mambo mengi kuhusu kuzaliwa kwa Kristo, moja ya haya ilikuwa kwamba yeye angeitwa Imanuel, inamaanisha "Mungu _____ _____"

4. Herode alikuwa mfalme wa Yuda ambaye alijaribu kumuua Yesu. Herode ali _____ watoto wote chini ya umri wa miaka miwili ambao waliishi katikati na kuzunguka Bethlehemu.

5. Mamajusi ambao walikwenda kumuona Yesu walikuwa wakifuata _____. Watu hawa walirudi nyumbani kwa njia tofauti na ile walioijia kwa sababu Mungu aliwaonya kupitia _____ kwa kuwa Herode alitaka kumuua Yesu.

6. Yusufu aliondoka na familia yake katikati ya usiku hadi Misri kwa sababu Mungu alimuonyesha Yusufu katika _____ kwamba Herode alikuwa akimtafuta Yesu.

7. Yusufu alijua kwamba ilikuwa salama kurudi Israeli kupitia _____. Lakini Yusufu hakurudi Bethlehemu, badala yake alichukua familia yake katika mji unaoitwa _____.

8. Jinsi Mungu alivyokwisha fanya popote katika historia, leo hii Mungu bado anatunza _____ zake.

9. Mungu anaelewa ni nini iko katika _____ yetu, hata ikiwa kuna wingi wa uovu pale.

10. Inawezekana kuwa mtu wa dini, hata kujua mengi kuhusu Biblia, lakini bado kamwe hajamjua _____ mwenyewe katika maisha yake.

"Tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia" Mathayo 3:2.

Haya yalikuwa ni maneno ambayo yalihubiriwa na mtu ambaye angeonekana katika jangwa la Yuda. Mtu huyu alivalia singa za ngamia na mshipi wa ngozi. Aliishi kwa kula asali ya porini na nzige. Jina lake aliitwa Yohana Mbatizaji.
Watu wengi kutoka maeneo yote yanayozunguka mto Yordani wangetoka kwenda Jangwani kusikiliza maneno yake. Kisha baada ya kumsikiliza yeye akisema. Wengi wangebatizwa katika mto wa Yordani wakiziungama dhambi zao. Wengi viongozi wa dini, wale walioitwa Wasadukayo na Wafarisayo, wangetoka nje kuona ni nini kilichokuwa kinatokea huko jangwani. Wakati Yohana Mbatizaji alipowaona, aliwaita wao, "Wazao wa Nyoka" akiendelea kusema kwamba hawakumuogopa Mungu kwa sababu walijidhania wenyewe kuwa ni wanadini na wa urithi mzuri. Kwamba wao hawahitaji kutubu dhambi zao.

Wakati Yohana alipokuwa akihubiri, Yesu alikuja na kumuuliza Yohana ambatize Yesu. Yohana hakutaka kufanya hivyo kwa mara ya kwanza kwa sababu alifikiri kuwa alikuwa hastahili kabisa kumbatiza Yesu. Lakini Yesu akakazana, na wote wawili wakaingia katika maji ya mto Yordani. Wakati Yesu alipopanda juu kutoka majini. Roho Mtakatifu alishuka kama hua kutoka mbinguni na akatua juu yake. Vile

vile, sauti kutoka mbinguni ikasikika ikisema, “Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.”

Baada ya hayo Roho mtakatifu akamchukua Yesu huko jangwani ili ajaribiwe na Shetani. Yesu alifunga kula chakula na maji kwa siku arobaini mchana na usiku, na baada ya siku hizo arobaini Yesu alishikwa na njaa. Ilikuwa ndio wakati huo ndipo Shetani alikuja kumjaribu yesu.

Biblia hutuambia juu ya majaribu matatu ya Yesu katika jangwa. Katika jaribu la kwanza, Shetani alijaribu kumfanya Yesu ageuze mawe yawe mkate, akidai kuwa hii ingedhihirisha kwamba Yesu alikuwa Mungu. Yesu alimjibu Shetani kwa kutumia Neno la Mungu lililoandikwa. Pili, Shetani alimpeleka Yesu katika paa ya hekalu na akamwambia Yesu kuruka na kujitupa chini ili kudhihirisha kuwa Yesu alikuwa Mungu. Lakini Yesu alimjibu Shetani vile vile akitumia Neno la Mungu lililoandikwa. Mwishoni, Shetani alimsafirisha Yesu juu ya mlima na akasema, “Haya yote nitakupa wewe ikiwa wewe utaanguka na kunisujudia mimi.” Yesu akamjibu Shetani akisema, “Msujudie Bwana Mungu wako na yeye peke yake ndiye utakayemtumikia.” Kwa haya Shetani akamwacha Yesu, na malaika wakaja wakamtumikia.

Baada ya kurudi kutoka Jangwani, Yesu alisikia kwamba Yohana Mbatizaji alikuwa ametupwa Gerezani. Kisha Yesu alikwenda Galilaya, mkoa ulio kaskazini mwa Yuda, akiuacha mji wa utotoni mwake, Nazareti, na kusogea Kaperanaumu. Hii ilikuwa ni utimilifu wa yale yaliyosemwa na nabii Isaya wakati aliposema, “Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, kwa njia ya bahari, ng’ambo ya Yordani, Galilaya na mataifa: watu wale wamekaa katika giza wameona nuru kuu na wale waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti nuru imewaangazia.”

Biblia hutuambia sisi kwamba kutoka mji huu Yesu alianza kazi yake miongoni mwa watu. Ujumbe ambao Yesu alihubiri ulikuwa ni huu “Tubuni kwa maana ufalme wa Mungu umekaribia.”

MASWALI YA MDOMO

1. Elezea mtu aliyeitwa Yohana Mbatizaji.
2. Ujumbe wa Yohana Mbatizaji ulikuwa ni nini?
3. Yohana Mbatizaji alifanya nini na wale walioziungama dhambi zao?
4. Kwa nini Yohana Mbatizaji hakutaka kumbatiza Yesu?
5. Kulitokea nini wakati Yesu alipopanda juu kutoka majini?
6. Ni kwa nini Yesu alikwenda nyikani?
7. Yesu alikaa bila nini kwa siku arobaini mchana na usiku?
8. Ni nini iliyokuwa mojawapo ya majaribu ya Shetanai?
9. Ni wapi Yesu alipokwenda baada ya kuarifiwa kuhusu kufungwa kwa Yohana Mbatizaji?
10. Yesu naYohana Mbatizaji walikuwa na ujumbe wa namna moja. Ulikuwa ni nini?

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 3-4

1. Ujumbe wa Yohana mbatizaji na wa Yesu ulikuwa mmoja, “Tubuni kwa maana ufalme wa Mungu unakaribia.”

♦ **Kutubu maana yake ni kugeuka kutoka dhambini katika maisha yako. Ina maana kutoa utawala wa maisha yako yote kwa Yesu Kristo, ukimruhusu yeye kuziondosha dhambi hizi.**

♦ Kwa nini sisi tunahitaji kutubu? Biblia inasema kwamba sisi sote tuna dhambi katika maisha yetu. **Dhambi ni kule tu kutomtii Mungu na sheria zake.** Kwa mfano, Biblia inasema kwamba kuua, kuiba, uongo, kiburi, tamaa na mifano mingine yote ni kutotii.

♦ Je, kutubu ni kitu kigumu kwa mtu kukifanya? Neno hili lina maana gani kwako? Jadili wazo hili miongoni mwa wajumbe wote wa kikundi. Umruhusu kila mmoja kuwa na nafasi ya kusema maoni yake.

2. Viongozi wa kikundi walijidhania kwamba wao hawahitaji kutubu juu ya dhambi zao kwa sababu ya dini yao. Wao walifikiria walikuwa wema vya kutosha. Yohana aliwaita watu hawa, “wana wa nyoka.” Je, kuna yeyote katika dunia ambaye ni

mwanadini tosha au hata wema vya kutosha ambao hawahitaji kutubu kwa ajili ya dhambi zao?

Biblia inasema katika Warumi 3:23 kwamba, "Wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."

- Je, kuna yeyote katika dunia ambaye hana dhambi katika maisha yake? Je, kuna yeyote ambaye kamwe hajawahi kutomtii au kuvunja utaratibu wa mwenendo wa Mungu au nia? Biblia inasema, "Hapana." Je, wewe unakubaliana na Biblia kwamba sisi sote tuna dhambi katika maisha yetu?

- Vile vile, ni muhimu kuruhusu kila mtu kuwa na nafasi kutaka kuthibitisha maneno ya Mungu juu ya swala hili. Kama kiongozi, usileta ubishi au kuruhusu yeyote alete ubishi, lakini ni sawasawa kuruhusu watu kusema mawazo yao.

3. Yesu alibatizwa, lakini yeye akiwa Mungu kamwe hakufanya dhambi.

Hii inatuambia sisi kwamba ubatizo sio utaratibu wa kidini ambao unaweza kuondoa dhambi kutoka maisha ya mtu. Ikiwa kusudi la ubatizo lilikuwa ni kusafisha mtu kutoka dhambini, Yesu asingelibatizwa kwa sababu yeye akiwa Mungu kamwe hakufanya dhambi.

4. Wakati Yesu alipoinuka kutoka majini, Roho Mtakatifu alishuka juu yake kama hua na Mungu Baba alizungumza kutoka mbinguni akisema, “Huyu ni mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.” Hapa tunaona zile nafsi tatu za Utakatifu. Ni zipi hizo?

Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu.

5. Yesu alipelekwa nje huko jangwani ili akajaribiwe na Shetani. **Shetani ni kweli yupo. Yeye ni roho ambaye yumo katika ulimwengu, pamoja na wengi wa wafuasi wa roho yake wakiitwa mapepo na wanaweza kuleta uharibifu kwa maisha yetu kutuongoza sisi kutomtii Mungu.** Kama Yesu alivyojaribiwa, Shetani vivyo hivyo anatujaribu pia na sisi. Biblia inatufundisha kwamba sisi, kinyume cha Kristo, pia tunajaribiwa kwa sababu ya uovu wetu ambao tayali unakuwako katika mioyo yetu kufanya mambo ya ambayo hayampendezi Mungu au dhambi.

6. Nabii Isaya alibashiri kwamba Yesu angekuwa nuru kuu watu wanao kaa gizani, sambamba na wale ambao wanaishi katika kivuli cha mauti.

Sisi sote, bila Kristo, tuko Gizani, lakini huenda wewe au mtu mmoja unayempenda anaishi katika kivuli cha mauti. Baadhi hujikuta pale kwa sababu ya madawa ya kulevya, wengine kupitia

uhusiano wa ki-uzinzi, na bado wengine ni madhubuti kwa utumiaji wa nguvu. Mstari huu gizani na yeye anaweza kutoa uhuru kwa wale ambao wanaishi katika kivuli cha mauti.

- Katika muda wetu wa maombi siku ya leo, ebu tuombe kwa ajili ya wale wapendwa ambao wanaishi katika kivuli cha mauti. Tuombe tupate nuru na uhuru katika Yesu kristo.

MIUJIZA YA YESU
MATHAYO 4-9

SOMO LA 3

"Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu." Mathayo 4:19

MARUDIO:

1. Ni nani aliyemuambia Yusufu kuhusu kuja kwake Yesu, na ni nani alimuambia kwamba jina lake lingekuwa "Imanueli" au "Mungu pamoja nasi"? Hii inatufundisha sisi kwamba Yesu ni _____ pamoja nasi.

2. Ni nani aliyetaka kumuua Yule mtoto mdogo Yesu? Kwa nini? Yesu alinusurika kwa wao kukimbilia _____.

3. Ni nani aliyembatiza Yesu? Ukweli kwamba Yesu alilazimika kubatizwa unatuambia sisi kwamba kazi ya ubatizo sio ondoleo la _____ katika maisha yetu.

4. Wakati Yesu alipotoka katika maji, kitu kama hua kilishuka chini toka mbinguni, na sauti vile vile na ilisikika kutoka mbinguni. Ni nani

aliyekuwa hua na sauti ya nani iliyokuja kutoka mbinguni?

5. Mafarisayo walifikiria kwamba wao hawakuhitaji kutubu kwa ajili ya dhambi zao kwa sababu wao walikuwa wanadini sana. Je, inawezekana kwa mtu kuwa mwanadini tosha kuondosha dhambi zake?

6. Ni nini maana ya neno kutubu?

7. Dhambi ni nini?

8. Ni nani aliyemjaribu Yesu jangwani

9. Yesu alikwenda wapi baada ya kutoka jangwani?

Wakati Yesu alipokuwa akitembea kando kando ya bahari ya Galilaya, aliwaona wavuvi wawili, Yesu aliwaita wao na kuwaambia, “Nifuateni nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu” mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata. Ilikuwa hapo ndipo Yesu aliwaita wanafunzi wake wane wa kwanza: Petro, Andrea, Yakobo na Yohana. Wote hawa walikuwa wavuvi. Kisha Yesu aliendelea kuzungukia mkoa mzima wa Galilaya akifundisha katika masinagogi, akihubiri injili ya ufalme, na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna miongoni mwa watu. Makutano makubwa yalimfuata popote Yesu alipokwenda.

Mtu mwenye ukoma alimjia Yesu na kuanza kumsujudia. Alimwita Yesu akisema, “Bwana ukitaka waweza kunitakasa.” Yesu akajibu, “nataka, kukutakasa.” Na mara ukoma wake ukatakasika.

Akida mmoja wa jeshi la Roma alimjia Yesu. Huyu bwana alikuja kumuuliza Yesu amponye mtumishi wake aliyekuwa na ugonjwa wa kupooza na anaumwa sana. Huyu akida aliamini katika uweza wa Yesu kumponya yule mgonjwa. Yesu alimwambia kwamba watu wengi wa mataifa yote wangekuja kula pamoja katika ufalme wa mbinguni na yule mtumishi wake akapona saa ile ile.

Wakati mwingine, kwa upande mwingine wa bahari, kulikuwepo na watu wawili waliokuwa na pepo. Watu hawa walikuwa na nguvu na wakali kiasi kwamba hakuna mtu wa kuwadhibiti au hata mtu asiweze kupitia njia ile waliokuwa. Waliishi makaburini. Wakati walipomuona Yesu, pepo walipiga kelele, “Tuna nini na wewe, Ewe Mwana wa Mungu? Je, umekuja kututesa kabla ya muhula wetu?”

Mbali kidogo na mahali walipokuwa kulikuwa na kundi la nguruwe. Wale pepo walimuomba Yesu “Ukitutoa, tuache twende tukaingie katika lile kundi la nguruwe.” Yesu akawaambia “Nendeni” pepo mara moja walifukuzwa kutoka kwa watu na wakaingia katika nguruwe. Wale nguruwe

wakageuka wakapagawa na pepo na kuwa wenda wazimu. Waliteremka chini kwa fujo na kwa kasi mteremko mkali wakajitosa baharini. Nguruwe wote walizama.

Wale wamilki wa wale nguruwe walikimbia na kuwaambia wenyeji wote wa mjini mwote kile Yesu alichokifanya, ikiwa ni pamoja na yale yaliyotokea kwa wale waliokuwa na pepo. Watu wa mjini walitoka kwenda kumlaki Yesu na kumsihi aondoke mkoani humo.

Yesu aliondoka kwa mtumbwi, akirudi mjini kwao. Mara baadaye, Yesu alikutana na mtu jina lake Mathayo. Mathayo alikuwa mtumishi wa serikali kama mtoza ushuru. Yesu alimwambia Mathayo, “Nifuate mimi.” Mathayo akasimama mara moja na kumfuata.

Kisha Yesu na wanafunzi wake walikwenda kula chakula cha usiku pamoja na watoza ushuru na watu wengine waliokuwa na sifa mbaya katika mji huo. Wakati viongozi wa dini, mafarisayo, walipoona hivi, waliwauliza wanafunzi wa Yesu, “mbona mwalimu wenu anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi?”

Wakati Yesu aliposikiwa maoni haya, aliwaambia Mafarisayo, “Wale wenye afya hawahitaji tabibu, bali wale walio wagonjwa, lakini nendeni mkajifunze maana

yake maneno haya. Mimi nataka rehema, wala sio sadaka. Kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.”

MASWALI YA MDOMO

1. Mwanafunzi wa kwanza wa Yesu alikuwa na kazi gain?

2. Walifanya nini wakati Yesu alipowaita kumfuata yeye?

3. Yesu alikuwa akienda kila sehemu ya Galilaya na makutano yalikuwa yakimfuata yeye. Alikuwa anafanya nini kuvuta usikivu kuja kwake?

4. Shida ya mtumishi wa Akida wa Kirumi ilikuwa ni nini?

5. Wale watu wenye pepo waliishi wapi? Walikuwa ni watu wa aina gani?

6. Pepo walifanya nini walipomuona Yesu?

7. Kulitokea nini kwa pepo wakati walipowaacha wale watu?

8. Kulitokea nini kwa nguruwe?

9. Wale watu wenye nguruwe walichukua hatua gani?

10. Mathayo alikuwa ni mtu wa aina gani?

11. Yesu alikula chakula cha jioni na watu wa aina gani?

12. Mafarisayo walifikiria nini juu ya hili?

13. Ni aina ya jibu ambalo Yesu alilitoa kwa Mafarisayo?

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 4-9

SOMO LA 3

1. **Yesu huwa hafanyi tofauti baina ya aina mbali mbali za watu.**

- Wanafunzi wa Yesu wa kwanza walikuwa ni wavuvi, watu wa kawaida, wasio nna elimu ya shule.

- Mwenye ukoma alikuwa mtu ambaye alikuwa ametengwa kutoka kwa jamii kwa sababu ya ugonjwa wa ngozi ambao ulimuacha umemharibu umbo na kudharauliwa.

- Mtumishi wa Akida wa Kirumi alikuwa ni kiwete, mtu ambaye hana pesa au nafasi yoyote katika jamii.

- Mathayo alikuwa mtoza ushuru. Hii ina maana kwamba alikuwa tajiri sana, lakini mwizi, mla-rushwa.

- Wale watu waliokuwa na pepo walikuwa wakidharauliwa na wananchi wenzao kwamba wale watu wa mjini walithamini nguruwe zilizonona kuliko kuponywa kwa watu hawa.

Kwa hakika watu hawa walikuwa wakiishi makaburini.

Watu wote hawa walikuwa wa muhimu na wathamani kwa Yesu. Wewe ni mtu wa thamani na unathaminiwa katika macho ya Mungu. Mambo yako yaliyopita, mambo yako ya fedha; kuonekana kwako katika jamii hakuna maana yoyote kwa Mungu.

2. **Yesu anao uwezo wa kuponya magonjwa yetu.** Upi mfano mmoja katika masimulizi haya ambaye aliponywa?

3. **Yesu anayo mamlaka juu ya pepo na mizimu.** Wapo watu wengi wamekuwa wakijihusisha na pepo au mizimu, mara nyingi kwa sababu wao wanajaribu kufanya mambo ambayo ni mazuri. Lakini kabla wao hawajajua ni kipi kilichotokea kwao, pepo hawa wameisha chukua maisha yao. Wao hufuatwa na kuteswa na pepo hawa ambao kamwe hawaachii wao pekee. Watu hawa hawana uwezo wa kuwadhibiti pepo hawa kutoka kwa maisha yao. **Yesu anayo mamlaka na uwezo juu ya kila pepo na mzimu katika ulimwengu. Sisi tunaweza tukawa nao uhuru kutoka kwa roho wachafu kupitia kwa Yesu Kristo pekee.**

4. **Yesu anawapenda watu wote hata wale ambao wanazo sifa mbaya. Yeye huwakubali wote.** Yesu huwa hawahukumu watu, lakini shauku

lake ni kuleta kila mtu kutubu na kupata msamaha wa kweli.

5. Watu wanadini au Mafarisayo, hawakutubu juu ya dhambi zao, na walifikiri kwamba wao ni bora zaidi kuliko watenda dhambi ambao walikuwa wanakula pamoja na Yesu. **Ni lipi lililo jema: kuwa na mtu mwenye dhambi ambaye ameishi samehewa, au mtu aliye na dhambi si nyingi lakini ambaye anakataa kutubu?**

♦ Ni bora kuwa na mtu mtenda dhambi ambaye ameisha samehewa.

Yesu anatukubali sisi na anatupenda sisi jinsi tulivyo. Haidhuru kwake ikiwa sisi ni watenda dhambi wa ajabu, ikiwa sisi tu maskini, ikiwa sisi tunayo elimu ndogo, ikiwa sisi tunayo matatizo mengi au ikiwa tunayo maumivu ya kimwili (maradhi). Katika macho yake, sisi sote tuko sawa. Kitu muhimu ni juu yetu kutubu na kumfuata yeye.

MAFUNDISHO YA YESU
MATHAYO 10-16

SOMO LA 4

"Nataka Rehema na wala si sadaka" Matnayo 12:7

MARUDIO

1. Yesu alizaliwa na mwanamke Myahudi jina lake _____.

2. Mamajusi kutoka mashariki waliweza kumuona Yesu kwa sababu walikuwa wanafuata _____.

3. Mamajusi hawakurudi kwa makao ya Herode kwa sababu walikuwa wameonywa na Mungu katika _____ kurudi nyumbani kwa kupitia njia nyingine.

4. Yohana Mbatizaji aliishi katika jangwa akihubiri na _____ wale watu ambao waliungama dhambi zao.

5. Nini maana ya neno "kutubu"?

6. Wakati Yesu alipobatizwa _____ alishuka

ulimwengu kama hua na sauti kutoka mbinguni ikasema. Hii inatudhihirisha sisi zile nafasi tatu za Mungu: Mungu _____, Mungu _____ na Mungu _____ _____. Sisi tunauita huu ni Utatu Mtakatifu.

7. Katika jangwa, Yesu alijaribiwa na _____.

8. Wanafunzi wa kwanza wa Yesu walikuwa wanafanya kazi ipi?

9. Yesu alikutana na watu wawili waliokuwa na pepo. Jinsi gani Yesu alivyowasaidia watu hawa? Jinsi gani watu wa mjini walivyochukulia tendo la Yesu

10. Mafarisayo walimsunta Yesu kwa sababu alikula pamoja na watu wa aina gani?

11. Je, ni bora mtu mwenye dhambi ambaye ameisha tubu au mtu aliye na dhambi chache na hakuna kutubu?

Yesu aliwaita watu kumi na wawili kuwa wanafunzi wake. Hii ina maana kwamba watu hawa walikuwa wawe karibu naye na kufunzwa na yeye. Yeye aliwapa hawa watu kumi na wawili uwezo juu ya pepo chafu, na uwezo wa kuponya magonjwa ya kila aina. Yesu aliwaambia wafuasi wake kwamba wao ni lazima watoe bure, kwa

sababu wamepata bure. Na Yuda Iskarioti alikuwa miongoni mwa watu hawa ambao walitumwa nje.

Yesu aliwatuma wao kila kona ya nchi ya Israeli ili kusudi kuwaita Wayahudi kutubu na kuwa na imani katika Kristo Yesu. Yesu aliwapa watu hawa ujumbe, "Kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, yeye, Nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Lakini yeyote atakayenikana mbele ya watu nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni."

Yesu mweyewe vile vile alitembea Galilaya yote akifundisha, akihubiri na kuponya magonjwa ya aina zote. Lakini kwa watu wa Galilaya, ambao walishinda pamoja na Yesu waliukataa ujumbe wake. Mji wa kaperanaumu, mahali alipoanza huduma yake kwa umma, walimkataa yeye. Kwa kuona haya Yesu alikwenda faragha kuzungumza na Baba yake, na haya ndiyo yaliyokuwa maneno yake,

"Nashukuru wewe Baba, Bwana wa mbingu na nchi kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili ukawafunulia watoto mbele zako. Nimekabidhiwa vyote na Baba yangu, wala hakuna amjuaye Mwana, ila Baba. Wala hakuna amjuaye Baba ila Mwana, na yeyote ambaye Mwana apenda kumfunulia. Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu, kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu,

nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi."

Baada ya kusema mambo haya, Yesu na wanafunzi wake walipita katika mashamba ya ngano. Hii ilikuwa ni siku ya Sabato au siku ya Wayahudi kupumzika. Wanafunzi wa Yesu walikuwa na njaa, hivyo walisimama, wakaanza kuvunja masuke na kula.

Mafarisayo, kumbuka hawa walikuwa ni viongozi wa dini, waliona jambo hili na wakawashitaki wao kwa sababu ilikuwa ni kinyume cha sheria za Kiyahudi kufanya kazi siku ya sabato. Yesu alijibu kwa kusema kwamba wao bado hawajaelewa ile sheria ya Mungu kwa sababu Maandiko Matakatifu yanasema, "Nataka rehema na wala sio sadaka."

Kutoka kwa mashamba ya ngano, Yesu na wanafunzi wake walienda kwa Sinagogi la Kiyahudi na pale wakamkuta mtu aliyepooza mkono. Yesu alimwambia yule mtu kuunyoosha nje mkono wake, na Yesu akamponya yule mtu pale pale ndani ya Sinagogi mbele ya wote siku hiyo ya Sabato.

Wale Mafarisyao, wakaudhika, wakaondoka sehemu ile na wakaunda baraza ili wakafanye shauri baya ya Yesu na kumuua yeye. Yesu hali akijua ni kitu gani wao walichokuwa wakipanga, pia akaondoka mahali pale. Lakini watu wengi

wakamfuata yeye. Hivyo alipowaponya wote na akawakataza wasimdhihirishe.

Hivyo Yesu aliendelea kufanya kazi katika mkoa huu muda kitambo kidogo akiwafundisha watu na kuponya magonjwa yao. Mara mbili watu walimfuata Yesu nje katika nyika ambako walikaa kwa muda mrefu wakisikiliza maneno yake hadi Yesu akawa na wasiwasi kwamba wasingeweza kurudi majumbani bila ya kula. Mara mbili, Yesu alichukua pungufu ya mikate saba na samaki wachache na kuwalisha zaidi ya watu elfu nne.

Bado angali anafanya kazi katika Galilaya, Yesu aliwaeleza wazi wafuasi wake kwamba punde karibu angekwenda Yerusaremu, na mambo ya kutisha yangetokea.

Yesu aliwaambia wafuasi wake kwamba yeye angepata mateso mengi kutoka kwa wazee na wakuu, mikononi ya viongozi wa Kiyahudi, kwamba angeuawa, lakini kwamba siku tatu baadaye angefufuka tena.

MASWALI YA MDOMO

1. Yesu aliwapatia wanafunzi wake jukumu gani?
2. Yesu alisema kwamba angefanya nini kuhusu wale ambao walimkana yeye mbele za watu?

3. Jinsi gani wenyeji wa Kaperanaum, sambamba na miji mingine mingi katika Galilaya, mahali Yesu alifanya miujiza mingi, walivyouchukulia ujumbe wake?

4. Yesu alisema kwa wale wote ambao wanasumbuka na kulemewa na mizigo kuja kwake. Anaahidi kufanya nini kwa ajili ya watu hawa?

5. Ni kwa nini Yesu na wanafunzi wake walisimama katika shamba la ngano?

6. Ni kwa nini Mafarisayo walimsuta Yesu kwa kukusanya ngano?

7. Ni kwa nini Mafarisayo hawakumuunga Yesu mkono alipomponya yule mtu aliyekuwa na mkono wa kupooza?

8. Nini lililokuwa kusudi la baraza lililoundwa na viongozi wa Kiyahudi?

9. Yesu aliwaambia wafuasi wake kwamba mambo fulani yalikuwa yamtokee yeye. Unabii wake ulikuwa upi?

KWELI ZA KIROHO

MATHAYO 10-16

SOMO LA 4

1. **Wale ambao wanalikiri jina la Yesu mbele za watu, Yesu atamkiri mbele za Baba yake.** Kwa hali ile, wale ambao wanamkana Yesu mbele ya watu, yeye naye pia atawakana mbele ya Baba yake huko mbinguni.

2. **Watu wengi walimfuata Yesu kwa sababu tu wao walitaka baadhi ya miujiza kutoka kwake; lakini hawakutaka uhusiano nay eye. Wao hawakutaka kutii maneno yake.** Wao hawakutaka kutubu dhambi zao. Wao walitaka tu kufurahia rehema za Mungu. Wao walikuwa wakimtaka Kristo pale tu walipomhitaji au wakati wao walipotaka kitu fulani kutoka kwake. Leo hii je bado wapo watu wengi wa jinsi hii? Wewe unafikiriaje juu ya jambo hili?

3. Mtu pekee aliye na njia ya kwenda kwa Baba ni Yesu Kristo na wale ambao wanakuja kwa Baba kupitia Yesu Kristo. **Hakuna njia mmoja tu na ipo njia moja tu ya kumfikia Mungu, na Biblia hutufundisha kwamba njia hiyo ni Yesu Kristo.**

♦ Huenda wewe umekuwa ukifundishwa kuomba Mungu kupitia wapatanishi wengine mbali na Yesu Kristo. Hawa wapatanishi wengine ni akina

nani? Je, wao ni miungu, manabii, watu wema wa kale? Biblia inasema huenda walikuwa watu wema, lakini wao sio Mungu. Je, wewe unaafikiana na Biblia kwa yupo mpatanishi mmoja tu kati ya Mungu na mwanadamu, Yesu Kristo

4. **Yesu anataka kubeba mizigo yetu na taabu zetu. Yeye ni mpole na mnyenyekevu wa moyo.** Yeye anataka kutupunguzia uzito ambao tunaubeba. Tunapata raha nafsini mwetu ikiwa sisi tutakubali nira yake. Katika maneno mengine, ikiwa tutakubali Ubwana wake au uongozi wake katika maisha yetu, kuna raha.

5. **"Nataka rehema na si sadaka"** Neno sadaka lina maana gani kwako wewe? Je, umewahi kufundishwa na viongozi wa dini kutengeneza sadaka kwa Mungu, huenda iwe ni kwa ajili ya kupata upendeleo au msamaha wa ndambi? Je, inakuwa vigumu kwako kuamini kwamba Mungu hataki wewe kuhakikisha kitu chochote kwake kwa sadaka zako au kwa kufanya tendo la huruma kwake? Je, haujawahi kufikiria kuhusu ukweli kwamba sisi hatuwezi kumpendeza Mungu, kumlipa Mungu au kutuliza Mungu kutokana na tendo la kidini, idadi yoyote ya pesa au baadhi ya tendo la sadaka? Hii ni mara ya pili ambapo yesu alijaribu kuwaeleza Mafarisayo kwamba Mungu hapendezwi na sadaka zetu za kibinadamu. Lakini kwa wale watu ambao ni wanadini sana, mara nyingi kwao inawawia

vigumu. Kuukubali ukweli huu. Dini zote zinafundisha kwamba lazima sisi tufanye kitu ili kusudi kukwepa hasira za Mungu au kupata upendeleo wa Mungu. Watu wengi hupitia katika shida nyingi wakijaribu kumlipa Mungu kwa ajili ya ahadi walizozifanya, kulipia kwa ajili ya dhambi za zamani au tu kuonyesha uaminifu kwa Mungu. Lakini hii haimaanishi chochote kwa Mungu. Yeye anataka uhusiano na sisi. Yeye anataka kutuonyesha sisi rehema, yeye hataki sadaka zetu.

6. Yesu alijua kwamba itamlazimu kuteseka mambo mengi na kisha kufariki. Lakini baada ya siku tatu, yeye angefufuka katika wafu. Hii ilikuwa yote ni sehemu ya mpango wa Mungu. Yesu alijaribu kueleza jambo hili kwa wanafunzi wake, lakini hawakuweza kuelewa ni kwa nini ilikuwa lazima Yesu afe na kasha afufuke.

♦ Katika mafundisho matatu ya mwisho ya somo hili, tutajaribu kuelewa maana ya kifo cha Yesu na ufufuo. Tukio hili, ni moja la aina yake na lingebadili historia ya ulimwengu milele. Tukio hili moja lina nguvu za kuvunja utumwa wa dhambi na kubadili maisha yetu.

KUZALIWA KWA YESU
MATHAYO 20-26

SOMO LA 5

"Hata Yesu alipokuwa akipanda kwenda Yerusalemu, aliwachukua wale wanafunzi kumi na wawili faraghani; na njiani akawambia, Angalieni tunapopanda kwenda Yerusalemu; na mwana wa Adamu atatiwa mikononi mwa wakuu makuani na waandishi; nao watamhukumu afe; kisha watampeleka kwa mataifa wapate kumdhihaki, na kumpiga mijeledi na kumsubili. Na siku ya tatu atafufuka" Mathayo 20:17-19.

MARUDIO

1. Yesu alizaliwa na bikira jina lake _____.

2. Baba yake wa ki-dunia_____, alikuwa na ndoto, ambayo katika hiyo ndoto, Mungu alimwambia Yeye akimbilie Misri kwa sababu Mfalme Herode alitaka _____Yesu.

3. Yohana Mbatizaji aliishi jangwani akihubiri na kubatiza wale wote _____dhambi zao.

4. Yesu hakuwa na _____ yoyote, lakini alimsisitiza Yohana Mbatizaji kumbatiza.

5. Neno “kutubu” lina maana gani?

6. Wakati Yesu alipobatizwa _____ _____ alishuka kama hua na sauti ya Mungu ilisikika ikisema, “Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninaye pendezwa naye.”

7. Katika jangwa, Yesu alijaribiwa _____.

8. Yesu alikutana na watu wawili waliokuwa na _____ Yesu alidhihirisha kwamba Yeye anao uwezo wa _____pepo.

9. Kipi kilicho bora, kuwa mtu mtenda dhambi lakini anayetubu au kuwa mtu mwenye dhambi chache na kamwe kutokutubu.

10. Yesu alisema kwamba ikiwa wewe utamkiri Yeye mbele za watu, yeye naye atakukili wewe mbele ya _____ yake wa mbinguni.

11. Wagalilaya wengi, wakiwemo wenyeji wa mji wa kaperanaumu _____ Neno la mungu, wao tu walimfuata Yesu kwa sababu ya miujiza mingi aliyoifanya.

12. Wao hawakutaka kutubu zambi zao . Tena,neno “kutubu” lina maanagani?

13. Yesu alisema kwamba yeye angetoa _____ kwa wale wote wanao

sumbuka na kulemewa na mizigo kwa kuwa nira yake ni nyepesi.

14. Mafarisayo walikuwa na mpango wa _____Yesu.

15. Yesu alijua kwa Mfarisayo walikuwa wakipanga kifo chake, lakini Yeye bado aliendele kufanya miujiza mingi ikiwemo kuzidisha _____wawili na_____ kulisha zaidi ya watu elfu nne.

Yesu pamoja na wafunzi wake, Walifanya safari kutoka Galilaya hadi Yerusalemu. Yeye alivyokuwa anakalibia kufika katika Yerusalemu, Yesu aliwambia wanafunzi wawili kati ya wanafunzi wake kupita kijiji fulani wamlete punda na mwana- punda ambao Yeye aliwahgitaji. Yesu akaketi juu ya mwanapunda huyu kwa safari ya kuingia mjini Yerusalemu.

Yeye aliingia kwa utukufu mwingi na shangwe kuu. Watu wengi walikusanyika na kumzunguka kila upande wa bara bra. Idadi kubwa ya watu ilitandaza nguo zao wenyewe njiani ili kutengeneza kitu kamajamvi kwa ajili ya Yesu kuingia katika mji. Wengine wakakata matawi ya miti na kuyatandaza pote njiani kama jinsi ya kumheshimu yeye. Bado wengine walikuwa wakitembea wengine mbele na wengine wakimfuata nyuma wakipaaza auti, “Hosana kwa

Mwana wa Daudi, ndiye mbarikiwa yeye ajaye kwa jina la Bwana? Hosana juu mbinguni!"

Mji mzima wa Yerusalemu ukataharuki kwa tukio hili kubwa na la aina yake. Kila mmoja katika mji alikuwa akiuliza, "Ni nani huyu?" Watu wengi sana wakasema, "Huyu ni Yesu, nabii kutoka Nazareti ya Galilaya."

Hivyo Yesu akaingia mjini akaenda kwenye Sinagogi la Wayahudi. Pale aliwatimua nje wachuuzi wote; yeye alizipindua meza wabadili fedha ambao walikuwa wakiuza na kununua hekaluni. Akawaambia wao, "Imeandikwa, nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala, bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi." Baada ya tukio hili, alikaa hekaluni akiwaponya vipofu na viwete.

Baada ya Yesu kuwafundisha watu mambo mengi na kufanya maajabu katika hekalu, wakuu wa makuhani na viongozi wa dini waliungana pamoja ili kwamba kupanga njama ya kifo chake. Wao walijadiliana njia ambayo wao wangemuua Yesu. Wao walikuwa kwa hali yoyote, wenye mashaka kuhusu utekelezaji wa mpango huo wakati wa pasaka – ikiwa ni siku kuu muhimu ya kidini, hivyo waliamua kusubiri mpaka Pasaka ipite ndipo wamshughulikie Yesu.
Sasa mmoja wa wale wanafunzi, yule mmoja anayeitwa Yuda Iskarioti, alikwenda kukutana na wakuu wa makuhani akasema, "Ni nini

mtakachonipa ikiwa nitamsaliti kwenu?" Wao walikubali na wakampa vipande thelathini vya fedha. Na tokea wakati huo ndipo Yuda akaanza kutafuta nafasi ambapo angeweza kumsaliti Yesu.

Ilikuwa juma la Pasaka, wanafunzi waliandaa chakula cha mchana kwa ajili ya sherehe kufuatana na maelezo maalum yaliyotolewa na Yesu. Usiku ule wa sherehe, Yesu aliketi pamoja na wale thenashara na aliwaambia, "Amini nawaambia ninyi, mmoja wenu atanisaliti" Jinsi alivyosema hivi, wale wanafunzi wakahuzunika sana na wakaanza kumuuliza mmoja mmoja, "Bwana ni mimi?"

Yesu akawaajibu wao akasema, "yeye aliyetia mkono wake pamoja nami katika kikombe ndiye atakayenisaliti. Mwana wa Adamu kweli aenda zake kama ilivyoandikwa juu yake, lakini ole wake mtu yule ambaye amsaliti Mwana wa Adamu! Ingekuwa heri kwake mtu yule kama asingezaliwa."

Yuda aliyekuwa anamsaliti Yesu akauliza, Rabda ni mimi? Na Yesu akamjibu Yuda, "Wewe umesema."

Kisha wakala chakula wao wote pamoja jioni ile na walipokuwa bado wanakula, Yesu alitwaa mkate, akabariki, akaumega akisema, "Twaeni mle: huu ndio mwili wangu." Kisha akakitwaa

kikombe, akashukuru na akawapa wao akisema, “Nyweni nyote katika hiki. Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya Agano Jipya, imwagikayo kwa ajili yaw engi kwa ondoleo la dhambi.”

Baada ya kumaliza chakula, waliimba wimbo, na kwa pamoja kasha wakaenda mlima wa Mzeituni. Huko Yerusalemu aliendelea kuwafundisha wao maombi mengi ambayo baadhi yalikuwa yakihusiana na matukio ambayo yalikuwa pende yatokee.

Baadaye usiku ule, Yesu aliwaleta wao mpaka mahali panaitwa (Gethsemane mahali ambapo walikuwa wafanye maombi pamoja nayeye kwa muda wote uliobakia wa usiku. Basi Yesu akamchukua Petro, Yakobo na Yohana pamoja na yeye na akaanza kusononeka. Akawaomba wao tafadhari wakae pale pamoja na yeye. Yeye kasha akawaacha wao na akaendelea mbele kidogo kuomba kwa Baba yake akiwa pekee. Maneno yake yamenukuliwa kama ifuatavyo:-

“Baba yangu, ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke, walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe.”

Imeandikwa kwamba Yesu aliomba sara hii mara tatu na moyo wake ulikuwa na hudhuni nyingi kiasi cha kufa.

Wanafunzi, kwa kadiri yoyote, hawakuweza hata kukaa macho kwa saa moja wao wote walilala usingizi. Mwishowe, Yesu aliwaamusha wote akiwaambia. “Amka, twendeni zetu. Tazama, msaliti wangu amekaribia.”

MASWALI YA MDOMO

1. Yesu aliingia Yerusalemu akiwa ameketi juu ya mnyama wa aina gani?

2. Watu walimtembeleaje Yesu alipokuwa akiingia katika mji?

3. Yuda alifanya nini kumsaliti Yesu?

4. Ni sikukuu ipi iliyokuwa inasherekewa katika mji?

5. Jinsi gani Yesu alivyomonya Yuda kwamba yeye anajua kwamba anamsaliti?

6. Yesu alisema nini kuhusu Divai wakati wa chakula cha jioni?

7. Kufuatana na Yesu, kumwagika damu ni lazima kwa ajili ya nini?

8. Yesu aliwachukua wanafunzi wake hadi Gethsemane kutumia usiku mzima katika

maombi. Ni wangapi kati ya hao wanafunzi waliweza kukesha usiku mzima wakiomba?

9. Ilikuwa ni sara ipi ambayo Yesu aliomba ule usiku wa kusalitiwa kwake?

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 20-26

SOMO LA 5

1. **Mungu ni mtawala wa vitu vyotte.** Mafarisayo walikuwa wanafanya njama za kumkamata Yesu kwa mashangao. Lakini Mungu, kwa muda wote, alikuwa akiwatumia wao kutenda mapenzi ya Mungu kwamba yesu angekufa juu ya msalaba.

2. **Mungu anajua yale yaliyomo mioyoni mwetu hata kama wengine hawajui.** Yesu alijua kwa muda wote kuwa mwanafunzi wake, Yuda, alikuwa anakwenda kumsaliti.

3. **Yesu anatupenda sisi na anatutendea sisi upendo ule ule hata ikiwa sisi tunamkataa yeye.** Yuda alitendewa vyema mno na Yesu kiasi kwamba hakuna mwanafunzi ambaye angeamini kwamba Yuda alikuwa ni msaliti. Katika njia

hiyo hiyo, Yesu anatupenda sisi na anatutendea sisi kwa upendo hata ingawaje mara nyingi tumemsaliti na kumkataa yeye na mapenzi yake kwa ajili ya maisha yetu.

4. **Damu ya Yesu ilimwagika kwa ajili yetu kwa kulegeza au msamaha wa shambi zetu.** Wanafunzi kwa wakati huo, hawakuelewa ukweli kwamba Yesu ingemlazimu kufa. Wao hawakuelewa kwamba Mungu anadai kwa kila mtu malipo ya dhambi katika maisha yao na kwamba malipo haya ni kumwagika kwa damu. Wao walielewa kwamba Yesu anawapenda wao na kwamba wao walikuwa wamesamehewa juu ya dhambi zao. Lakini wangehitaji muda zaidi mpaka wameelewa thamani ambayo Yesu ilibidi alipe ili kuweza kusamehe dhambi zao.

♦ Watu wengi wanajua kwamba wanazo dhambi katika maisha yao. Baadhi ya watu huenda wamewahi kusikia hadithi ya Yesu, na kwamba yeye anawapenda. Lakini wachache sana wanaelewa kwamba Mungu anadai sadaka ya damu kama malipo kwa ajili ya dhambi. Yesu kwa sababu yeye ni Mungu, ndiye mtu pekee ambaye aliwahi kuishi au atakayeishi juu ya ulimwengu huu bila ya kuwa na dhambi hata moja na mmoja pekee au kitu ambacho kingekubaliwa kama sadaka – badala kwa ajili ya dhambi zetu. Kwa sababu ya upendo wake usiopimika kwa ajili Yetu sisi, yeye alichagua kutoa maisha yake ili yawesadaka ya kulipa

thamani kwa dhambi zetu na sio tu kwa dhambi zetu mbali kwa ajili ya ulimwengu wote. Ni kwa sababu ya sadaka hii, ambapo sisi sasa tuna nafasi ya kupokea msamaha kwa ajili ya dhambi na amani na Mungu.

Juma lijalo, sisi tutaangalia kwa maelezo kusulubiwa kwa Kristo.

KUSULUBIWA KWA YESU
MATHAYO 26-27

SOMO LA 6

Yesu akamwambia kuhani mkuu, "Wewe umesema, lakini nawaambieni tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni" Mathayo 26:64.

MARUDIO

1. Yesu alizaliwa na bikra ambaye jina lake lilikuwa _____.

2. Kama Maandiko Matakatifu yalivyokwisha sema, Yesu alikimbilia kwenye nchi ya _____, kwa sababu yeye alikuwa anakimbia kutoka Mfalme Herode.

3. Baba wa kidunia wa Yesu _____ alikuwa na ndoto ikimshauri yeye kurejea Israeli baada ya mfalme Herode kufariki.

4. Yesu alianza huduma yake kwa umma kwa kubatizwa na _____ _____ _____.

5. Wakati Yesu akitoka majini _____ _____ kama hua alikuja chini kutoka mbinguni, vile vile sauti ya _____

ilisikika kutoka mbinguni ikisema, “Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.”

6. Yesu aliwaponya watu wengi na kuwasamehe juu ya _____ zao.

7. Hata baada ya miujiza mingi, watu wengi kutoka mkoa wa Galilaya _____ ujumbe wa Yesu, na hawakutaka kutubu juu ya dhambi zao.

8. Nini maana ya neon “kutubu”?

9. Wakati Yesu alipokwenda katika mji wa Yerusalemu, kulikuwa na maandamano makubwa ya watu waliomfuata yeye. Katika maandamano hayo, Yesu alikuwa ameketi juu ya _____.

10. Usiku ule wa sherehe za Pasaka, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba mmoja wao ange _____ yeye. Kwa wakati ule hakuna mtu aliyejua ni nani kati yao.

11. Yesu alizungumzia divai waliyokuwa wanakunywa. Yeye alisema kwamba iliwakilisha damu yake ambayo ingemwagika kwa ajili ya _____ la dhambi.

12. Wale wanafunzi waliyasikia maneno haya lakini bado hawakuweza kuelewa kwamba Yesu

alikuwa anakwenda ku _____ kwa ajili ya dhambi zao.

13. Baada ya chakula cha mchana, wao wote walikwenda hadi Mlima wa Mizeituni na baadaye hadi Gethsemane. Yesu aliomba wakati wa usiku ambapo wanafunzi wake walikuwa _____.

14. Yesu aliomba "Ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke, walakini si kama nitakavyo mimi bali kama _____."

Wakati Yesu alipokuwa bado angali anawaamsha wanafunzi wake, yule aliyemsaliti, alifika pamoja na kundi kubwa la watu wakiwemo wakuu wa makuhani na viongozi wa dini wengi wakiwa wamebeba mapanga na marungu. Yuda alimwendea Yesu na akambusu akisema, "Salamu Rabi." Yesu akamjibu Yuda, "Rafiki kwa nini umekuja"?

Ghafla, mmoja wa wanafunzi wa Yesu, kwa haraka aliuvuta upanga na akakata sikio la mmoja wa watumishi wa kuhani mkuu. Yesu aliita usikivu wa wanafunzi wake na akamponya yule mtu sikio lake. Yesu alimtaarifu huyu mwanafunzi kwamba ikiwa Yesu angetaka kulikuwa na majeshi kumi na mawili ya malaika walio tayari kupambana, lakini yote hayo yaliyokuwa yanatokea yalikuwa ni mapenzi ya Baba ili Maandiko yatimike.

Kisha Yesu akaligeukia lile kundi la watu lililokuwa limewasili na kuwauliza “Je, mmetoka kama kumkamata mnyang’anyi, wenye panga na marungu ili kunishika mimi? Kila siku niliketi pamoja na ninyi, nikifundisha hekaluni na wala msinikamate. Lakini haya yote yamekuwa ili Maandiko Matakatifu ya manabii wengine yatimizwe.”

Na wanafunzi wake haraka wakamwacha wakakimbia kutoka mahali pale, Yesu akabaki peke yake.

Hivyo wale ambao walimkamata Yesu, wakamchukua kwa nyumba ya mtu aliyeitwa Kayafa ambaye kwa wakati ule alikuwa Kuhanani Mkuu. Kwa kuwa penye nyumba ya Kayafa ndiko waliokuwa wamekutanika makuhani wote na viongozi wa dini tayari kwa kumhoji Yesu.

Walikuwa wameisha waandaa mashahidi wa uongo, kutoka ushahidi dhidi ya Yesu ili waweze kumhukumu kifo. Na hakika wengi walijitokeza, lakini hata hivyo hawakuweza kukusanya ushahidi wa kutosha wa kuweza kumhukumu kifo mpaka kuhani mkuu mwenyewe akaja kumhoji Yesu. Kayafa mwishowe akamuuliza Yesu, “Mimi ninakuapisha kwa Mungu aliye hai: Utuambie sisi ikiwa wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu!”

Yesu akamwambia Kayafa, “Wewe umesema lakini nawaambieni, tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu, ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni.”

Kuhani mkuu, kwa kusikia jibu hili, akararua mavazi yake akisema “Amekufuru.” Watu ambao walikuwa wamekusanyika pale ndipo wakamchukua Yesu na kuanza kumtemea mate juu ya uso wake. Wengine wakampiga makonde na baadhi wakampiga makofi wakisema, “Ewe Kristo tufumbulie ni nani aliyekupiga wewe?

Ilipofika asubuhi makuhani na viongozi wa dini wakamchukua Yesu kwa liwali wa kirumi wa mkoa aliyeitwa Pilato. Yesu alikuwa ameishatiwa hatiani katika mahakama yao ya kidini wao, kanisa walikuwa hawana mamlaka ya kumsulubisha yeyote yule. Wao walimueleza Pilato kwamba Yesu alidai kuwa ndiye Mfalme wa Wayahudi, hivyo wamfanya kuwa na hatia ya ukaidi kwa serikali ya Roma.

Pilato akamchukua Yesu na kumhoji. “Wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi?” Yesu akamjibu, “Wewe wasema.”

Lakini hata baada ya mahojiano hayo yote, Pilato hakuweza kupata sababu yoyote ya kumsulubisha Yesu. Vile vile, usiku wa kabla, mke wa Pilato alikuwa na ndoto iliyomsumbua kuhusu swala

zima na akamuonya mumewe ili asiwe na chochote cha kufanya juu ya Yesu. Pilato alijua kwamba viongozi wa Kiyahudi walikuwa wamemleta Yesu mbele yake kutokana na ushuhuda. Lakini Pilato hakujua afanya nini kwa watu ambao watu ambao walichochewa pamoja nay ale yote yaliyokwisha tokea.

Kila mwaka, wakati wa pasaka, imekuwa ni desturi ya liwali kumfungulia mfungwa mmoja ambaye ni chaguo la watu. Mwaka huu, kulikuwa na mfungwa mashuhuri katika gereza aliyeitwa Baraba. Basi Pilato akawatoa Baraba na Yesu na akatoa nafasi kwa watu.

Ni nani mnayemtaka mimi niwafungulie ninyi? Baraba au yesu anaitwa Kristo? Lakin wale watu ambao walikuwa wamechochewa hasira na Mafarisayo wakapaaza sauti “Baraba!” Basi nimtendeje Yesu aitwaye Kristo? Pilato aliuliza. Watu wakasema “Mwache Yesu asulubiwe.”

Basi Pilato alipoona watu wanaanza kufanya ghasia, akachukua bakuli la maji na akanawa mikono yake akisema, “Mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki, yaangalieni haya ninyi wenyewe mijeredi.

Askari wa Liwali wakamchukua ndani ya Praitorio, makao makuu ya Pilato, huko wakamtesha na kumdhihaki. Wao wote wakamkusanyikia, wakamzunguska, wakamvua

nguo, wakamvika vazi jekundu. Wakasokota taji ya miiba, na wakaiweka juu ya kichwa chake. Wao walimpa Yesu mwanzi kushikilia katika mikononi mwake, kana kwamba ilikuwa ni fimbo na wakapiga magoti mbele yake wakimdhihaki wakisema, “Salaamu Mfalme wa Wayahudi.” Walimtemea mate kasha wakautwaa ule mwazi ambao ulikuwa mikononi mwake na kumpigapiga kichwani na mwazi huo. Baada ya kumaliza kufanya yale waliyoyafafnya, wakamvua lile vazi, wakamvika mavazi yake, na wakamchukua mahali panapoitwa Golgotha au “Fuvu la kichwa.” Hapa ni mahali ambapo Yesu alikuwa asulubiwe. Yesu aliulubiwa hapo, na juu ya msalaba, wakaweka kibao juu ya kichwa chake kilichoandikwa maandiko yanayosema “Huyu ni Yesu mfalme wa Wayahudi.”

Yesu alisulubiwa katikati ya majizi wawili, mmoja upande huu na mwingine upande mwingine wa Yesu.

Wakati Yesu alipokuwa akining’nia juu ya msalaba, tokea saa sita hadi saa tisa, Yesu alilia akisema Eloi, eloi, lama sabakthani? Yaani Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Na baadaye kidogo Yesu alipaza sauti tena. Ilikuwa ni wakati wa kupaaza sauti huku ndipo Yesu akaiachilia Roho yake.

Wakati ule Yesu alipoitoa Roho wake, mambo mengi ya ajabu yalitokea. Pazia la hekalu

lilipasuka vipande viwili toka juu hadi, chini ikitetemeka, miamba mingi ikapasuka na makaburi mengi yakafunuka, ambapo miili mingi ya watakatifu waliolala wakainuka. Miili hii baada ya ufufuo wake wakiisha kutoka makaburini mwao waliingia mji wa Yerusalemu na walionekana na watu wengi.

MASWALI YA MDOMO

1. Jinsi gani Yesu alivyosalitiwa?

2. Mmoja wa wanafunzi wa Yesu alifanya kitu fulani katika jitihada za kumlinda Yesu. Ilikuwa ni nini na Yesu alichukuliaje tendo hilo?

3. Wakati wa kusalitiwa kwake Yesu, wanafunzi wake wote walifanya nini?

4. Watu walipotoka bustanini walimpeleka Yesu wapi?

5. Hata hivyo, ingawa palikuwepo na mashahidi wengi wa uongo, jinsi gani hatimaye walivyomtia Yesu hatiani kwa kukufuru?

6. Viongozi wa Kiyahudi walimpeleka Yesu wapi mara baada ya asubuhi kuanza?

7. Pilato baada ya mahojiano yake, hakumkuta na hatia yoyote Yesu lakini aliwaogopa watu, hivyo aliwapa watu chaguo. Nini ilikuwa toleo alilowapa watu na chaguo lipi la watu?

8. Maaskari walimtendea vipi Yesu?

9. Baada ya masaa matatu ya giza, Yesu alipaza sauti kwa Mungu kulitokea nini kwa Roho wake wakati alipopaza sauti?

10. Ni mambo gani baadhi yaliyotokea katika Yerusalemu wakati Yesu alipoitoa Roho yake?

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 26-27

SOMO LA 6

1. Yesu yu nani? **"Mwana wa Adamu aliyekaa mkono wa kuume wa nguvu na anayekuja juu ya mawingu ya mbinguni."** Hili lilikuwa ni jibu ambalo Yesu alilotoa kwa kuhani mkuu, na lilikuwa ni jibu ambalo hatimaye lilielekeza kwenye kusulubiwa kwake. Lilikuwa ni jibu ambalo wale watu hawangelikubali. Kila mtu aliyezaliwa juu dunia hii lazima apambane na swali hili hili. Yesu hasa ni nani? Ilikuwa Yesu hasa amekaa mkono wa kuume wa nguvu na anayekuja juu ya mawingu ya mbinguni, ni lazima kila mmoja aamue jinsi gani tutakavyo chukulia kuja kwake.

2. Yesu alisulubiwa mahali pa Baraba, mhalifu mashuhuri; na Baraba kama badala yake aliachiliwa huru.

♦ Huenda mimi sio mhalifu mashuhuri, lakini kama vile Baraba, mimi ni mtenda dhambi na mbele ya Mungu mimi pia ninastahili hukumu ya kifo. Biblia inasema katika Warumi 6:23 **"Mshahara wa dhambi ni mauti."** Hii ina maana kwamba sisi sote tunastahili kifo kwa sababu ya mambo mabaya ambayo tumefanya katika maisha yetu. Haidhuru ikiwa tunazo dhambi nyingi kama vile katika shauri la Baraba, au ikiwa sisi tumekuwa na uhusiano na watu wema kama baadhi ya wanafunzi wake walivyokuwa.

3. **Yesu aliteswa, alihukumiwa na kuuliwa kwa kulipa adhabu kwa ajili ya dhambi katika maisha yetu.** Hii ilikuwa ndiyo sababu iliyomleta Yesu duniani. Mungu hudai kwamba kila mmoja wetu alipe kwa ajili ya dhambi ambazo tumezitenda. Yesu amelipa deni hili kwa sababu alitaka sisi tuweze kusimama mbele za Mungu tukiwa tumesamehewa juu ya dhambi zetu. Baadhi ya watu wamesema kwamba Yesu mwenyewe. Yesu alidai kuwa Mungu na alikuja ulimwenguni ili kufa kwa ajili ya dhambi zetu.

4. **Yesu alitoa Roho Wake.** Kwa muda wake wowote Yesu angekuwa ameshuka kutoka msalabani. Yeye angeweza kuua wale watu wote waliomfanyia vituko kwa neon moja. Lakini kwa kuchagua Yeye mwenyewe, alivumilia fedheha na akakaa msalabani mpaka saa ilipotimia. Ndipo wakati kazi yake hapa ilipomalizika, yeye aliachia Roho yake. Yeye alichagua kufa kwa sababu yeye alitaka kulipa deni kwa ajili ya dhambi zetu. Biblia inasema katika Yohana 3:16 kwamba, “Mungu aliupenda ulimwengu kwamba yeye alitoa Mwanae pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa Milele.”

♦ Katika fundisho linalofuata tutajifunza kufufuka kwa Yesu. Kwa kuwa kweli ni kwamba Yesu sio mfu, bali yuko hai na leo hii anataka kuingia ndani ya maisha yako. Yesu anataka kutakasa moyo wako kutoka kwa

dhambi zako zote na kubadilisha maisha yako kabisa.

- *Kiongozi – ikiwa wewe unajisikia una faraja na ikiwa Roho anakuongoza, unaweza kutoa mwaliko wakati wa kufunga kikao hiki.*

UFUFUO WA YESU
MATHAYO 27 – 28

SOMO LA 7

"Msiogope ninyi kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulubiwa. Hayupo hapa, kwani amefufuka kama alivyosema" Mathayo 28:5-6

MARUDIO

1. Yesu alizaliwa na msichana Bikira jina lake _____

2. Yesu alianza huduma yake kwa umma kwa _____ na mtu mmoja aliyeitwa Yohana Mbatizaji.

3. Penye ubatizo wake _____ _____ alishuka juu yake kama hua, na sauti ya Mungu ilisikika kutoka mbinguni ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa _____ ninaye pendezwa naye." Hii inatuonyesha sisi zile nafsi tatu za Utatu Mtakatifu: Mungu _____, Mungu _____ na Mungu _____ _____.

4. Yesu aliponya watu wengi magonjwa yao na aliwasamehe watu wengi _____ zao.

5. Hata baada ya miujiza mingi, watu wengi ambao waliishi katika Galilaya walikataa maneno ya Yesu na hawakutaka _____ juu ya dhambi.

6. Neno “Kutubu” Lina maana gani?

7. Yesu alisema kwamba divai inawakilisha damu yake ambayo ingemwagika kwa ajili ya wengi kwa _____ ya dhambi.

8. Mafarisayo walimkataa Yesu katika bustani mahali ambapo alipokuwa akifanyia maombi, na wakampeleka kwa nyumba ya _____ Mkuu ambaye jina lilikuwa ni Kayafa.

9. Kuhani mkuu alimuuliza Yesu ikiwa yeye ni _____ na Yesu akajibu kwamba yeye alikuwa ndiye. Kwa wakati huu watu walikuja kwa Yesu na _____ katika uso wake, _____ yeye, na wakampiga Yesu kwa viganja vya mikono yao.

10. Wakati wa asubuhi ulipowadia, mafarisayo walimpeleka Yesu kwa Liwali wa Kirumi ambaye jina lake lilikuwa _____

11. Pilato hakupatwa na hatia yeyote, lakini aliruhusu Yesu kusulubiwa kwa sababu Pilato alihofia _____ miongoni mwa watu.

12. Askari wa Kirumi walimtesa Yesu. Waliweka taji la _____ juu ya kichwa chake na wakampigapiga kichwani kwa mwanzi ambao walikuwa wamempa Yesu kuushikilia.

13. Juu ya msalaba mahali Yesu alipotundikwa, kulikuwa na kibao kinachosema “Huyu ni Yesu _____ wa Wayahudi.”

14. Tokea sasa sita hadi saa tisa kulikuwa _____ juu ya ulimwengu.

Kulikuwa na mtu mmoja tajiri sana aliyeitwa Yusufu wa Arimathaya ambaye pia alikuwa ni mwanafunzi wa Yesu. Huyu mtu alimuomba Pilato ikiwa angeruhusiwa kuuchukua mwili na kumlaza Yesu katika kaburi jipya. Baada ya kumlaza Yesu pango, jiwe kubwa lilivingirishwa dhidi ya mlango wa kaburi.

Siku ya pili, mafarisayo walikutana pamoja na wakamwendea Pilato kwa sababu walikuwa ni wamekumbuka maneno ya Yesu wakati Yesu aliposema kwamba Yesu angefufuka tena siku ya tatu. Wao walimuomba Pilato ikiwa angefanya kaburi kulindwa mpaka siku ya tatu ikiwa jambo lolote lingetokea kwa mwili huo. Pilato aliwapa ruhusa kulilinda kama wao walivyojua. Wao wakaenda mahali pale, wakaweka walinzi mbele ya kaburi, na wakaweka muhuri kwa lile jiwe.

Siku ya kwanza ya juma, Maria Magdalena na Maria yule wa pili, walikwenda kaburini mahali Yesu alipokuwa amelazwa. Walipofika pale, kulitokea tetemeko la ardhi, lile jiwe lililowekewa mhuri kwenye lango la kaburi lilikuwa limeondolewa, na malaika wa Bwana alikuwa

amekaa juu ya jiwe lile. Walinzi ambao waliokuwa wakilinda kaburi walitetemeka na wakawa kama wafu. Lakini, malaika akawaambia wale wanawake akasema, “Msiogope ninyi kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulubiwa. Hayupo hapa, kwani amefufuka kama alivyosema. Njoni mpatazame mahali alipolazwa. Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake kwamba amefufuka, na hakika atawatangulia ndiko mtakakomwona. Haya nimekwisha waambia.”

Wale wanawake wakatoka mle kaburini wakiwa na hofu na furaha nyingi wakaenda mbio kuwapasha wanafunzi yale yaliyotokea. Lakini walipokuwa wangali wanakwenda kuwaona wanafunzi, Yesu alikutana nao akasema, “Furahini!” Wakasema, wakamshika miguu na wakamsujudia Yeye. Yesu aliwaambia wale wanawake, ili wawaambie wanafunzi wakutane nay eye huko Galilaya.

Basi wale maaskari waliokuwa wakilinda kaburi waliingia mjini na kuwapasha habari wakuu wa makuhani habari za mambo yaliyotokea kwenye kaburi. Wakuu wa makuhani walifanya shauri kusambaza habari mji mzima kwamba wanafunzi wameuiba mwili wakati walinzi walipokuwa wamelala usingizi mahali pale. Makuhani pia waliwaahidi wale walinzi kwamba ikiwa neno hili litamfikia Pilato kwamba walinzi walikuwa wamelala ndipo makuhani wenyewe watasema na Pilato kuwalinda maaskari mbele ya liwali. Basi askari wakapokea hongo na wakaeneza uvumi

mwingi ambapo ulienea kote mji mzima kwa miaka mingi.

Wanafunzi kumi na moja waliosalia walikwenda hadi Galilaya kwenye mlima mahali Yesu alikuwa ameisha waambia kukutana naye. Wakati walipomuona Yesu, wao wote walimsujudia yeye, lakini baadhi yao waliona shaka.

Hivyo Yesu akawaambia wanafunzi wake kwa mara ya mwisho akisema, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari. Amen.”

MASWALI YA MDOMO

1. Yusufu wa Arimathaya alimuomba Pilato nini?
2. Mafarisayo waliogopa kwamba kitu fulani kingetokea kwa mwili wa Yesu siku ya tatu. Kwa nini?
3. Ni nani aliyekwenda kumuona Yesu siku ile ya kwanza na hawa wanawake waliona nini wakati walipowasili penye kaburi?

4. Wakati walipokuwa wakirudi kuwaambia wanafunzi kile walichogundua, walijitupa kwa nani?

5. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwakuta wao mahali pengine mbali na Yerusalemu. Mahali hapo palikuwa wapi?

6. Juu yam lima Yesu alikuwa na amri iliyo muhimu sana ya kuwapa wanafunzi wake. Jaribu kujaza nafasi zilizo wazi kwa maneno ya Yesu: "Basi enendeni na mkawafanye mataifa yote kuwa _____, _____ wao katika jina la Baba, na Mwana na _____ _____, mkiwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 27-28

SOMO LA 7

1. Yesu yu hai leo hii. **Yesu sio mwanadamu ambaye anaweza kufungwa au kuuwa. Yeye ni Mungu wa milele.** Yesu hana mwanzo wala mwisho. Mungu tangia mwanzo wa ulimwengu ilikuwa kuja duniani katika umbo la kibinadamu kama mtumishi atesekaye. Ilikuwa ni mapenzi yake kusulubiwa siku ile na kwa jinsi hiyo. Mipango yake. Haiwezi ikazuilika, wala hakuna yeyote awezaye kushindana juu yake. Yeye bado siku zote atakuwa Mungu, Mungu pekee aliye hai.

2. Mafarisayo waliyaamini maneno ya Yesu kufika hatua ya kwamba ilibidi wawe na askari wa kulinda kaburi la Yesu baada ya kifo cha Yesu kwa sababu Yesu alikuwa ameahidi kufufuka tena. Wao waliamini maneno ya maaskari wakati walipoambiwa ni kipi kilichotokea. Wao hata walilipa wale maaskari kwa kuogopa kuhusu tukio hili. Baadhi ya viongozi wale wale walikuwa wamehudhuria, wakati Yohana Mbatizaji alipombatiza Yesu, na sauti ya Mungu mwenyewe ilisikika kutoka mbinguni ikithibitisha Yesu alikuwa nani. Wengine wa viongozi hawa walikuwa mashahidi kwa miujiza mingi ambayo Yesu aliifanya. Wao walikasirishwa na Yesu wakati Yesu alipomponya mtu mwenye mkono uliopooza ikiwa ni siku ya sabato. Wao walikuwa wamemuona Yesu akifukuza pepo

kutoka watu waliokuwa na maumivu makali, na wao walikuwa wamemwona Yesu akiwasamehe watu juu ya dhambi zao. Nusura pasiwepo mtu aliyejua zaidi kuhusu maisha na ujumbe wa Yesu kuliko walivyofanya Mafarisayo. Lakini kundi hili-hili la watu hawa kukubali Upendo wa Mungu ambao aliutoa katika maisha yao mwenyewe. Wao hawakutubu juu ya dhambi zao. Wao hawakutoa utawala wa maisha yao kwa mamlaka ya Yesu Kristo. **Kuwa na uhusiano na Yesu Kristo ni zaidi kuliko kujifunza na kuamini kweli za maisha yake. Ni zaidi kuliko dini mpya na iliyotofauti. Yesu anashauku kuona sisi tunatubu juu ya dhambi zetu, kuamini katika yeye na kumpa yeye maisha yetu. Yeye anataka kuwa Bwana au kiongozi wa maisha yetu. Yeye anataka kutawala sisi kila siku ya maisha yetu.**

3. Yesu ni nani?

- Yesu alizaliwa na bikra.
- Yesu alidai kuwa yeye alikuwa Mungu.
- Yesu alifanya miujiza mingi na aliwasamehe watu ambao walitubu juu ya dhambi zao.
- Yesu alikufa msalabani ili kulipa thamani kwa ajili ya dhambi katika maisha yetu mbele za

Mungu wa haki. Yesu alifufuka kutoka wafu na sasa yu hai.

- Yesu anataka mimi vilevile nitubu juu ya dhambi zangu na kutoa maisha yangu kwake.

  Biblia inatufundisha sisi kwamba Yesu hakufa ili awe mfano, alikufa ili awe badala yako na mimi ambao tunastahili kujieleza kwa Mungu kwa mambo yote ambayo tumefanya vibaya katika maisha yetu.

  Biblia inasema kwamba, "Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka" Warumi 10:13.

- Hii ina maana kwamba bila kujali mambo yangu yaliyopita ninaweza kumuomba Yesu kuja katika maisha yangu nay eye atanisamehe mimi juu ya dhambi zangu zote na kuishi katika maisha yangu.

- Ina maana kwamba tangu dakika ile Yesu anapoingia katika moyo wangu dhambi zangu zote za awali, dhambi za hivi sasa na dhambi zijazo ziko tayari zimeisha sameheka mbele za Mungu. Hii siyo kwa sababu ya kitu chochote ambacho nimefanya. Siyo kwa sababu mimi nimechagua dini nzuri. Siyo kwa sababu mimi nimekuwa mtu mwadilifu. Sio kwa sababu wazazi wangu wanatoka katika ukoo maarufu au daraja fulani katika jamii. Ni kwa sababu tu

nimekubali sadaka ambayo Yesu tayari amelipa wakati alipokufa msalabani.

- Ina maana kwamba kutoka dakika hii na kuendelea mimi ni mtu msafi tena katika mcho ya Mungu, sina hatia. Biblia inatufundisha kwamba mshahara wa dhambi ni mauti, lakini kifo cha Kristo kinatosha, kunifanya mimi kiumbe kipya. Ikiwa mimi ninachagua kumfuata yeye.

Ikiwa wewe ungependa msamaha wa Mungu hivi sasa katika maisha yako, na ungelipenda kuwa mfuasi wa Kristo wewe unaweza kuomba yeye kuja katika moyo wako dakika hii hii. Sio lazima kuwa katika sehemu maalum ya dini, sio lazima kusema maneno maalum au maneno ya kiini macho, ni muhimu tu wewe kuja mbele za Mungu na ukiri kwamba wewe unaamini kuwa Yesu ni Mungu na unataka yeye awe Bwana au mtawala wa maisha yako.

Wewe unaweza kuomba kama hivi:

“Baba, mimi ninajua kwamba mimi ni mtenda dhambi. Mimi ninaamini kwamba Yesu alikufa msalabani na akafufuka kutoka kaburini ili kuniokoa mimi kutoka kwa dhambi zangu. ninatubu juu ya dhambi zzangu zote. Ninakupa maisha yangu. asante kwa upendo wako kwa ajili yangu. Katika jina la Yesu. Amina.”

4. **Na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.**

   Biblia inasema katika Yohana 14:2, “Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi, kama sivyo ningewaambia. Ninakwenda kuandaa makao kwa ajili yenu. Na ikiwa nikienda kuandaa mahali kwa ajili yenu, nitakuja tena niwakaribishe ninyi kwangu; ili nilipo mimi nanyi muwepo pia.”

   Yesu alituahidi sisi kwamba kila yeyote anayetoa maisha yake kwake, atatumia umilele pamoja naye katika mahali panaoitwa mbinguni. Mbinguni ni makao ya Baba. Mara sisi tunapompokea Yesu katika umilele unaanza leo hii kwa sababu Yesu atakuwa pamoja na sisi hapa duniani, na wakati tutakapo fariki tutatumia umilele pamoja nay eye mbinguni.

   Upendo ambao Yesu anao juu yetu sisi ni kweli ni wa kudumu milele!

UKWELI WA INJILI HAUBADILIKI LAKINI MITAZAMO HUBADILIKA KULINGANA NA UTAMADUNI

KUMBUKA: Katika jamii ya kikristo unaweza kuendelea kutumia maswali ya milele. Lakini katika jamii ya wasio amini utatakiwa kutumia utambuzi katika kutambua kiwango cha uelewa wa kiroho. Uelewa wa mtu katika neno kama vile mbinguni linaweza kuwa ni tofauti na lile la kwenye Biblia.

Kuiwakilisha Injili

(Mistari sita inayoeleza ukuu wa injili.)

1. Kusudi la Mungu katika maisha yako

Biblia inasema katika I Yohana **5:13, "Nimewaandikia ninyi mambo hayo ili mjue ya kuwa mnao uzima wa milele ninyi mlioliamini jina la Mwana wa Mungu."**

Kusudi la mstari: Mungu anataka kutupa hakika ya maisha ya milele kwa sababu ya upendo wake kwa mwanadamu.

Maelezo ya mstari: Maisha ya milele ni vitu viwili:

a) Kumjua Yesu na kuwa na amani yake ktika moyo wako wakati ukiwa katika maisha haya. (Yohana 17:3)
b) Kuishi na Yesu Kristo mbinguni milele baada ya kufa (Yohana 14:1-3)

Matumizi ya Mstari: Unatakiwa kujua kwa uhakika kwamba unao uzima wa milele ?

Angalizo: Kwa Wakristo na wasio Wakristo maelezo haya yanatakiwa kuwa wazi kimaelezo na inaweza kukuchukua muda.

2. Hitaji lako

Biblia inasema katika **Warumi 3:23**, **"Wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu".**

Kusudi la mstari huu: Ni kuonesha kwamba wote wana dhambi.

Maelezo ya mstari: Dhambi ni nini? Dhambi ni kutomtii Mungu. Kwa mfano, wote sisi tumefanya dhambi kama vile uongo, hasira, urafi, majivuno n.k.

Matumizi ya mstari huu: Unatambua ya kwamba umefanya dhambi na ni nini madhara ya dhambi?

Biblia inasema katika warumi **6:23, "Mshahara wa dhambi ni mauti bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu."**

Kusudi la mstari: Unaonesha kwamba wote tunastahili mauti kwa sababu tumetenda dhambi.
Maelezo ya Mstari: mauti ni nini? Ina maana ya kutengana na Mungu katika njia mbili.

> Kwanza, mauti ni kutengana na Mungu sasa katika maisha ya duniani hapa. Ni maisha yasiyo na furaha au amani katika Roho. Ni maisha yasiyo na uhakika wa uzima wa milele na bila Yesu katika roho yako. Utengano wa Mungu

humwacha mwanadamu akiwa tupu na roho yenye woga.

Pili, mauti ni utengano na Mungu milele katika jehanamu. Haya ni maisha bila Yesu milele yote. Kulingana na Biblia sisi sote tunastahili mauti, na kutengana na Mungu kwa sababu ya dhambi zetu.

Matumizi ya Mstari: Unaelewa kwamba unastahili kufa kwa sababu ya dhambi zako?

3. Pendo la Mungu

Biblia inasema katika Warumi **5:8, "Bali Mungu aonesha pendo lake kwetu sisi wakati tungali wenye dhambi, Kristo akafa kwa ajiri yetu."**

Kusudi a mstari: kuonesha kwamba Mungu anatupenda sana hata akamtoa mwana wake Yesu Kristo akafa kwa ajiri ya dhambi zetu.

Maelezo ya mstari: Mshahara wa dhambi ni mauti. Yesu Kristo aliadhibiwa akahukumiwa na kuuawa msalabani ili alipe gharama ya dhambi zetu.
Kifo cha Yesu kilikuwa ni dhabihu kamili ili kumweka huru mwanadamu kutoka katika dhambi. Watu wengi wanajaribu kumfikia Mungu kwa njia nyingi: wakitegema kazi zao, maisha yao mazuri, Wanajaribui kumfikia Mungu kwa njia ya utakatifu, sanamu, michoro, roho chafu na wafu. Juhudi za mwanadamu hazina nguvu za kutakasa dhambi yake. Njia ya kuweka ushirika na Mungu ni kupitia Yesu tu. Baada ya Yesu

kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu, alifufuka kutoka wafu akayashinda mauti. Yu hai na anataka aingie na kuishi katika maisha yako.

Matumizi ya Mstari huu: Unaamini kwamba Yesu ni Bwana wako, Mwokozi na mpatanishi?

4. Jukumu lako

Biblia inasema katika Warumi **10: 9, "Kwamba ukimkiri Yesu kwa kinywa chako na kuamini moyoni mwako ya kwamba Yesu ni Bwana na kwamba Mungu alimfufua katika wafu utaokoka."**

Kusudi la mstari: Ni kukuonesha cha kufanya ili upate kumpokea Yesu kama Bwana wako
Maelezo ya mstari: Kumpokea Yesu unatakiwa kufanya mambo mawili:

a) Kwanza, Kumpokea Yesu unapaswa kukiri kwamba yeye ni Bwana wako tu. Uzikatae dhambi zako na ugeuke kumfuata Yesu. Hii inamaana kuacha kuendesha maisha yako na kumpa Yesu. Na hii ni toba

b) Pili, kumpokea Yesu unapaswa kuamini moyoni mwako kwamba Yesu alifufuka katika wafu na kwamba yeye ni mwokozi wako. Ina maana kwamba unapaswa kuacha kuamini mambo mengine kama vile kazi nzuri,vinyago, sanamu, utakatifu au wafu na uweke imani yako kwa Yesu kama Mwokozi wako .

Matumizi ya Mstari: Uko tayari kumkiri Yesu kama Bwana na mwokozi wako na umkabidhi maisha yako kama Bwana? Je uko tayari kuacha kuabudu vitu vingine na umpe Kristo maisha yako sasa kama Bwana na Mwokozi wako?

Biblia inasema katika Warumi **10:13, "Atakayeliitia jina la Bwana ataokoka."**

Kusudi la mstari: Ni kuonesha kwamba yeyote atakayeliitia jina la Bwana ataokoka.

Maelezo ya Mstari: Unaweza kumpokea Yesu sasa kwa imani katika moyo wako.

Matumizi ya mstari: Uko tayari kumkabidhi Yesu na umwombe aingie katika maisha yako sasa? Kama uko tayari sema sala hii kwa moyo wako mbele za Mungu.

> "Bwana, Mimi ni mwenye dhambi, ninakuamini Bwana, kama Bwana wangu tu, mwokozi na mpatanishi, ninayatoa maisha yangu kwako. Ingia katika moyo wangu na uniokoe sasa, nigeuze na uyaongoze maisha yangu yote. Amen."

Unaamini kwamba Yesu amejibu maombi yako? Umeokoka?